

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

TAASISI YA TAALUMA YA WANYAMAPORI - PASIANSI



SHINDANO LA UANDISHI WA INSHA – JUNI 2017

1. Katika kuendeleza maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori – Pasiansi, Bodi ya Ushauri katika kikao chake cha 68-3 kilitoa maelekezo kuhusu kuendelea na mashindano ya michezo pamoja na uandishi wa insha kama sehemu ya maadhimisho hayo. Kwa mantiki hiyo, Taasisi iliandaa matukio mawili, ambapo shindano la michezo (bonanza) lilifanyika tarehe 28/01/2017 na shindano la uandishi wa insha kwa wanafunzi litahitimisha tarehe 01/07/2017 wakati wa sherehe za mahafari ya 52 ya Taasisi.
2. Shindano la uandishi wa insha linalenga kuongeza maarifa kwa wanafunzi wa shule na vyuo, hususan Kanda ya Ziwa juu ya uhifadhi wanyamapori kuendana na mpango wa taifa wa maendeleo endelevu. Kipaumbele kimeelekezwa zaidi katika kufanikisha malengo ya maendeleo endelevu pamoja na Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umaskini, awamu ya pili.
3. Mada ya insha ni “Umuhimu wa Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori – Pasiansi na Uhifadhi Wanyamapori uliotukuka katika kuchochea mafanikio ya malengo ya maendeleo endelevu na Mpango wa Kukuza na Kupunguza Umaskini, awamu ya pili nchini Tanzania”.
4. Shindano lipo wazi kwa wanafunzi wa vyuo (vikiwemo vyuo vikuu), sekondari na shule za msingi zilizopo Kanda ya Ziwa ambao wanatakiwa kuandika insha yenye maneno kati ya 750 hadi 1,500. Washiriki watatakiwa kutafiti mada husika, kuandika na kuwasilisha insha zao na mwisho wa kupokea insha ni tarehe 01 Juni, 2017.

Insha zote zitumwe kwa anuani ifuatayo:

Mkuu wa Taasisi,
Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori – Pasiansi,
S.L.P 1432,
MWANZA.

Barua pepe: principal@pasiansiwildlife.ac.tz

5. Mkuu wa Taasisi ataunda jopo la wataalam watakaokuwa na jukumu la kufanya mapitio ya insha zote na kuchagua insha zenye ubora. Baada ya jopo hilo kukamilisha kazi hiyo, litawasilisha katika Bodi ya Ushauri ya Taasisi insha zilizoshinda ambapo washindi watapatiwa zawadi siku ya tarehe 01 Julai, 2017.

Vigezo na masharti katika shindano hili ni kama ifuatavyo:

- Insha haitakiwi kuzidi maneno 750 kwa shule za msingi, 1000 kwa sekondari na 1500 kwa vyuo/vyuo vikuu.
- Pale ambapo washiriki wana fursa ya kupata komputa, wanashauriwa kuchapa insha zao na kuziwasilisha katika mfumo wa nakala laini (soft copy) na ngumu za (hard copy).
- Washiriki watakaochapa insha zao watapaswa kusaini nakala ngumu (hard copy) kuhakikisha kwamba haziwezi kubadilishwa.
- Kudurufu (duplication) kazi ya mtu mwingine itapelekea insha iliyowasilishwa kutopokelewa.
- Insha inapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
- Ukurasa wa kwanza sharti uonyeshe majina kamili ya mshiriki (majina matatu) kama yalivyo katika kitambulisho cha taifa au cheti cha kuzaliwa; jinsi; shule/chuo/chuo kikuu; anuani sahihi ikonyesha mkoa, wilaya na barua pepe; saina pamoja na namba ya simu.
- Mada ya insha inapaswa kuandikwa juu ya ukurasa wa juu kabisa (cover page) na washiriki hawatakiwi kubadilisha mada husika.
- Insha zilizoandikwa kwa mkono zinapaswa kuandikwa upande mmoja wa karatasi ya A4 kwa nafasi ya sentimita mbili (kutoka juu, chini, kushoto na kulia mwa karatasi).
- Insha zilizoandikwa kwa mkono sharti ziwe zenye kusomeka vizuri.
- Wanafunzi wa Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi HAWARUHUSIWI kushiriki katika shindano hili.